

Septemba 2016

**“Maskani zako zapendeza kama nini, Ee Bwana wa majeshi! Nafsi yangu imeziona shauku nyua za Bwana, Naam, na kuzikondea. Moyo wangu na mwili wangu vinamlilia Mungu aliye hai.” Zaburi 84: 1–2.**



Mwezi huu nimekuwa nikisoma Zaburi 84. Ni Zaburi inayoleta uponyaji kwenye moyo wangu wakati moyo wangu unapohitaji matumaini na uponyaji. Napenda ukweli unaoelezwa na Zaburi hii katika safari ya matumaini.

Ni safari halisi iliyoandikwa kwa wakati mzuri kwa ajili ya Israeli: labda Suleimani alipokuwa Mfalme. Kila mwaka walisafiri kwenda Yerusalemu kwa ajili ya sherehe za wayahudi. Walisafiri kutoka pande zote za Israeli kuja kumuabudu Mungu hekaluni.

Tunaposoma Zaburi 84, tunaangalia ndani ya moyo wa mmoja wa wale waliosafiri kwenda Yerusalemu kuabudu.

Nafikiria jinsi walivyotamani kukaa mbele za Mungu. Nimekuwa najiuliza, “Ninatamani kukaa mbele za Mungu kwa kiasi gani? Nitafanya nini kuhakikisha napata muda wa kukaa na Mungu kila siku?”

Zaburi inatulazimisha kuangalia vitu tunavyovitamani. Unaweza kuongea au kuyaomba maneno ya Zaburi hii kama vile ni ya kwako mwenyewe? Unatamani kukaa mbele zake? Moyo wangu una njaa kwa ajili ya Mungu?

Hivi karibuni niliugua kwa siku chache, na nilitamani kuwa mzima tena ili kurejea katika shughuli zangu za kila siku. Nikapata changamoto ya kufikiria, “Nafsi yangu inapoumia, napokea uponyaji kwa kumtamani Mungu? Mioyo yetu inapoumia kwa maumivu au mateso, tunamkimbilia na kutamani uwepo wa Mungu kwa kiwango kikubwa zaidi?”

Mwezi huu tunapoombea wanawake wa Bulgaria, Kroatia, Ugiriki, na Slovakia, tumkabidhi mambo yote yaliyopo kwenye mioyo yetu na kuinua sauti zetu kwa kutamani zaidi na kuwa na njaa ya kumpata Mungu. Tunapoumia, tumtafute na kuamini kuwa yeye ni tabibu mkuu kwa ajili ya uponyaji wetu.

Kwenye kalenda yetu ya Oktoba, msisitizo wetu utakuwa kuwa na njaa kwa ajili ya Mungu. Tutasogeza maombi yetu ya kila mwaka pamoja na kufunga ili yaendane na Siku ya Wanawake ulimwenguni mwezi Machi 2017.

Na mfahamu upendo na uponyaji wake mwezi huu mnapotembea kwenye safari ya matumaini pamoja na Bwana.

Katika yeye mioyo yetu inashangilia,

Peggy Banks

Mkurugenzi wa Huduma wa Kimataifa

Project Hannah